HOTUBA YA MHE. SAIDI MECK SADIKI KAIMU MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA UHURU YANAYOFANYIKA VIWANJA VYA MNAZI MMOJA DAR ES SALAAM TAREHE 16 AGOSTI 2011

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa,
Mhe. Katibu wa CCM Mkoa
Wahe. Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dar Es Salaam
Katibu Tawala wa Mkoa,
Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama (M),
Wahe. Wabunge wa Mkoa wa Dar- Es- Salaam,
Viongozi wa Vyama vya Siasa,
Mstahiki Meya wa Jiji
Mameya wa Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke
Viongozi wa Madhehebu ya Dini,
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji
Wakurugenzi wa Manispaa za Mkoa wa Dar Es Salaam,
Makatibu Tawala wa Wilaya za Mkoa wa Dar Es Salaam
Viongozi wa Taasisi mbalimbali
Waandishi wa Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana,

Asalaam aleykum,

Ndugu Wananchi,

Awali ya yote napenda tuungane sote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda sisi na nchi yetu ya Tanzania tangu tupate uhuru 9/12/1961 hadi leo hii ikiwa ni miaka 50 tukiwa na amani.

Nchi yetu imeendelea kuwa na amani na utulivu hadi leo hii tunapofikia miaka 50 ya uhuru.

Ndugu Wananchi,

Katika kusherehekea uzinduzi huu wa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru, yatupasa kukumbuka juhudi kubwa iliyofanywa na Muasisi Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere aliyeshirikiana na wenzake katika harakati za kupigania uhuru wa nchi yetu. Hali ya nchi yetu ilikuwa katika utawala wa Ukoloni, mfumo uliojenga matabaka ya Ubepari, Ukabila na Unyonyaji. Kuondokana na hali hiyo ilihitaji uzalendo na uchungu wa nchi hii na ndipo kukawepomaamuzi ya kuanzishwa programu mbali mbali ikiwemo Azimio la Arusha, Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, Siasa ni Kilimo, Operation Vijiji, Kuunganishwa kwa TANU na ASP na kuzaliwa kwa CCM, Chama kushika Hatamu, kurejeshwa kwa Serikali za Mitaa, kuachia madaraka (kung'atuka) kwa viongozi kwa mujibu wa Katiba na nyinginezo.

Ndugu Wananchi,

Ni vema tukakumbuka tulipopata Uhuru 9/12/1961, Mkoa wa Dar Es Salaam haukuwepo, kilichokuwepo ulikuwa ni Mji wa Dar Es Salaam. Eneo la Mkoa wa Dar Es Salaam lote lilikuwa lipo ndani ya Mkoa wa Pwani.

Jina la Dar Es Salaam lilitokana na majilio ya wageni wa Kiarabu waliotokea pande za Persia, waliita Bandari Ur Salama, kwa lugha ya Kiswahili Bandari ya Salama na kihistoria Jiji hili limekaliwa na kutwaliwa na wageni wa aina mbalimbali.

Wajerumani ni miongoni mwa wageni watawala waliohamishia makao makuu ya Serikali yao kutoka Bagamoyo kuja Dar ES Salaam mnamo mwaka 1891ulipotawazwa kuwa mji mkuu wa Serikali. Dhumuni kuu lilikuwa kuitumia bandari salama kusafirishia mazao ya kibiashara kutoka bara hadi pwani.

Mwaka 1916 hadi 1961 nchi ya Tanganyika ilikuwa chini ya Utawala wa Waingereza.

Mkoa wa Dar Es Salaam ulianzishwa mwaka 1973 ukiwa na Wilaya tatu za Ilala, Kinondoni na Temeke. Kipindi hicho Serikali Kuu ilihodhi Madaraka (Madaraka Mkoani) ikiwa ni kusudio la Serikali kuongeza kazi ya Maendeleo na kuwezesha Mikoa kusimamia shughuli za maendeleo kwa karibu zaidi.

Aidha mara baada ya Uhuru mwaka 1962 Serikali za Mitaa za wenyeji zilizorithiwa kutoka katika Utawala wa kikoloni zilivunjwa na kuanzisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye mamlaka kamili ya utendaji na uwajibikaji kwa wananchi.

Ndugu Wananchi,

Tunao ushahidi wa ufanisi mkubwa uliopatikana katika uwepo wa Serikali za Mitaa kwani wananchi wenyewe wamekuwa wakishirikishwa katika kupanga, kuamua, kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa mipango yao.

Ndugu Wananchi,

Mwaka huu una umuhimu wa kipekee hasa kwa Historia ya nchi yetu ambayo itatimiza miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania bara. Tunayo mafanikio mengi ya kujivunia kutokana na matunda ya Uhuru. Mafanikio haya makubwa hatuna budi kuyafurahia na kuyasherehekea kwa namna ya pekee. Ni vigumu kuweza kuorodhesha maendeleo na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam katika kipindi cha miaka 50. Hata hivyo nichukue nafasi hii siku ya leo kueleza baadhi ya mafaniko yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na kueleza kwa kifupi hali ilivyokuwa kabla ya Uhuru na hali ilivyo hivi sasa.

Kihistoria nchi yetu ilipopata uhuru hapo ndipo mji wa Dar Es Salaam ulipata hadhi na hati ya kuwa Makao Makuu ya Serikali ya Tanganyika na iliendelea kuwa Makao Makuu ya Tanganyika Huru na hatimaye kuwa Makao Makuu ya Serikali ya Muungano wa Tanzania hadi mwaka 1972 wakati Serikali ilipoamua kuhamishia Makao Makuu ya Serikali mjini Dodoma. Jiji la Dar Es Salaam liliendelea kubaki kuwa maarufu kama Jiji kuu na kitovu cha biashara nchini Tanzania.

MATUNDA YA UHURU KATIKA MKOA WA DAR ES SALAAM

ELIMU:

Kabla ya Uhuru Mkoa wa Dar Es Salaam ilikuwa na shule za Msingi chache sana ambazo baadhi zilikuwa chini ya Wamissionari. Hadi mwaka 1960 Shule za Sekondari zipatazo 10 (kumi) ambazo ni hizi zifuatazo:

_St Joseph Boys Secondary School – Forodhani Sekondari
_Government Indian Secondary School-Azania Sekondari
-Devun Kura Arya –DA Girls Secondary School-Kisutu Sekondari
-H.H. Aga Khan Girls Secondary School- Zanaki Sekondari
-H.H. Aga Khan Boys Secondary School- Tambaza Sekondari
-Chopra Secondary School- Shaaban Robert Sekondari
-St Francis College- Pugu Sekondari
-The International Secondary School
-Kurasini Girls Secondary School

-Mzizima Secondary School_Aga Khan Mzizima Sekondari
-St Xavier Secondary School – Kibasila Sekondari
-Jangwani Girls Secondary School- Jangwani Sekondari

Aidha kulikuwepo na Chuo pekee cha Ufundi ambacho ni Dar Es Salaam Technical College.
Mara baada ya Uhuru kukajengwa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam – The University College of Dar Es Salaam(1961) na baadae kikajengwa Chuo Kikuu cha Elimu Chang'ombe – Dar Es Salaam College of National Education (1965).

Kutokana na takwimu hizo tunaona kwamba wakati wa nchi yetu inapata uhuru, Mkoa wa Dar es Salaam haukuwa na shule nyingi na hata vyuo.

Sasa hivi Mkoa wa Dar es Salaam unazo Shule za Sekondari 361kati ya hizo za Serikali ni 134 ndani yake 123 ni zile zilizojengwa kwa nguvu za wananchi/kata na za Binafsi zipo 159 pia tunavyo vyuo vingi ikiwemo Vyuo Vikuu 12 kati ya hivyo vya Serikali ni 6 na vya binafsi 6. Pia yapo matawi 3 ya vyuo vikuu ambvyo viko mikoani. Aidha Mkoa unavyo vyuo vingine 19 - hayo yote ni matunda ya Uhuru.

ZAHANATI

Hadi wakati wa Uhuru Mkoa wa Pwani ndani yake ikiwemo Dar Es Salaam ulikuwa na Hospitali moja (1) ikiitwa St Magreth ambayo sasa inaitwa Muhimbili.

Mkoa wa Dar Es Salaam ulipoanzishwa mwaka 1973 huduma za tiba na kinga zilitolewa katika Hospitli ya Muhimbili na Vituo vya Afya 13 ambavyo cha Serikali kilikuwa kimoja (1) na vya Binafsi 12 pia kulikuwa na Zahanati 115 ambapo 16 zilikuwa za Serikali na 99 za Binafsi, baadaye zimeongezeka Hospitali 3 za Wilaya za Mwananyamala (Kinondoni), Amana (Ilala) na Temeke (Temeke) na Muhimbili sasa imeendelea kuwa Hospitali ya Rufaa kuhudumia wagonjwa kutoka nchi nzima.

Hivyo kwa sasa Mkoa wetu una Hospitali 33 kati ya hizo nne (4) za Serikali, 25 za binafsi na Hospitali 4 ni za mashirika ya dini. Vituo vya Afya vilivyopo ni 32 ambapo vya Serikali ni 5, Binafsi 4 na mashirika ya dini 23.

Aidha Zahanati nyingi zilianzishwa baada ya Uhuru hadi sasa zimefikia 392 ambapo Zahanati 89 ni za Serikali, 296 ni za Binafsi na 7 ni za taasisi za dini.

MAJI

Huduma ya maji kwa wakazi wa Dar es Salaam, kwa kiasi kikubwa hutolewa na Mamlaka ya Maji Mjini Dar es Salaam (DAWASA) ambayo imewakodishia kwa mkataba Kampuni ya DAWASCO kuendesha huduma hiyo kibiashara.

Maeneo yasiyohudumiwa na mtandao wa DAWASA hupata maji kutoka katika miradi inayoendeshwa na Taasisi, Sekta binafsi na jumuiya za watumia maji kutoka vyanzo vya visima vifupi na virefu.

Hadi mwaka 2011, viko jumla ya visima vifupi 248 na virefu 1,116 vinavyotumiwa kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Jiji. Ili kuendelea kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, na miji mipya ya Kibaha na Bagamoyo kuna mpango wa kuchimba visima ishirini katika eneo la Mpera na Kimbiji ambavyo vitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita za ujazo milioni 250 kwa siku ifikapo mwaka 2013.. Mahitaji ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo ni mita za ujazo 450 million kwa siku.

Miradi hii ya maji imekuwa ikiendelea kubuniwa kwa miaka hamsini sasa baada ya uhuru kwa lengo la kukidhi mahitaji ya maji katika Jiji la Dar es Salaam kwani ongezeko la kasi la watu na makazi, viwanda na biashara ni changamoto zinazohitaji uimarishwaji wa upatikanaji wa maji ili kukidhi utoaji wa huduma bora ya majisafi na majitaka

MIUNDOMBINU

BARABARA, MAWASILIANO NA MAJENGO

Hadi wakati wa Uhuru Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na bara bara za lami zenye urefu wa km 155. Urefu huu unajumuisha barabara kuu pamoja na barabara za maeneo (area roads/streets) ambayo yalikuwa yameanza kuendelezwa kwa ajili ya makazi, maofisi pamoja na maeneo ya biashara.

Aidha, barabara kuu zilikuwa ni 4 ambazo ni barabara ya Kilwa, Pugu, Morogoro pamoja na Old Bagamoyo.
Barabara za Mkoa, Wilaya na barabara ndogo ndogo (feeder roads) zimeendelea kuongezeka kadri mji ulivyokuwa ukiendelea kukua. Mapungufu ya barabara yanayojitokeza yanatokana na sehemu kubwa ya Jiji kuwa katika maeneo yasiyopimwa na hivyo mji kuendelea kupanuka bila kufuata mpangilio na utaratibu wowotena hii inatokana na hivyo matengenezo ya barabara yamekuwa hayakidhi mahitaji na hii ndiyo sababu ya kuwepo kwa msongamano mkubwa wa magari katika barabara zote za Jiji la Dar es Salaam.

MATENGENEZO YA BARABARA KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM:

Barabara za Jiji la Dar es Salaam zilianza kuboreshwa kupitia katika mradi wa matengenezo ya barabara Kitaifa uliotekelezwa katika awamu mbili za “Intergrated Roads

Programme (IRP I & II)" kuanzia mwaka 1987 – 1992 pamoja na Highway Projects kuanzia mwaka 1982 – 1985.

Serikali ya Japan kwa kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (Japan Internation Cooperation Agency - JICA) ilianza kuboresha barabara katika maeneo mbalimbali ya Jiji kwa kutumia fedha za msaada kutoka kwa wananchi wa Japan. Mradi wa wa-Japan (Japanese Grant Aid) uliokuwa unaitwa "Dar es Salaam Roads Improvement and maintenance Project (DRIMP)"

Mtandao wa Barabara za Mkoa wa Dar es Salaam:

Mtandao wa barabara za Mkoa wa Dar es Salaam una urefu wa kilomita 2094.4 ambapo kati ya hizo TANROADS inasimamia na kuhudumia barabara zenye urefu wa Km 494.3 ambazo ni barabara kuu (Trunk roads) na barabara za Mkoa (Regional Roads). Barabara zilizobaki zenye urefu wa Km 1600.1 ni barabara viungo (District and Feeder roads) ziko chini ya usimamizi wa Halmashauri za Manispaa za Ilala (Km 429), Kinondoni (km 692.7), na Temeke (km 478.4).

Barabara zilizoko chini ya usimamizi wa Halmashauri za Manispaa pamoja na Wakala wa barabara (TANROADS)

Aidha kuna huduma nyingine za usafiri na usarishaji kama ifuatavyo:-

i. Reli za TRC na TAZARA
ii. Kiwanja kikubwa cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)

iii. Bandari ya Dar es Salaam ambayo ni bandari kuu Pwani ya Afrika ya Mashariki kwenye Bahari ya Hindi

Mpango wa matengenezo ya barabara:

Mkoa umeweza kufanya matengenezo maalum ya barabara mbalimbali kupitia TANROADS na Halmashauri za Jiji na Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke.

Hivi karibuni matengenezo maalum ya barabara yalifanyika katika maeneo mbalimbali ikwemo barabara za Mkoa za changarawe zilizojengwa kwa kiwango cha lami.

Miradi maalum inayotekelezwa ili kupunguza msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam

i. Ubungo Bus Terminal – Kigogo Round about kwa urefu wa (km 6.5)

ii. Kigogo Roundabout – Jangwani Twiga (2.74 km)

iii. Tabata Dampo Kigogo na Ubungo Maziwa – Mabibo External (Mandela 2.25 km)

iv. Jet Corner – Vituka Devis Corner (12.0 km)

v. Mbezi Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (14. 0km)

vi. Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (18 km)

vii. Old Bagamoyo Road, na Garder Road urefu (9.1km)

viii. Tanki Bovu – Goba (9.0 km)

ix. Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (2.6 km)

x. Kimara – Kilungule – External (Mabibo – Mandela (9.0 km)

xi. Mfereji wa maji kuanzia barabara ya Nyerere hadi Barabara ya Uhuru (Bungoni drain).

Mpango wa kuboresha Makutano kwa kujenga Fly overs katika Jiji la Dar es Salaam:

Msongamano wa Magari uliopo katika Jiji la Dar es Salaam kwa sehemu kubwa unatokana na makutano ya Barabara kuzidiwa na wingi wa Magari. Ili kuondoa kero hii, mpango kabambe ulioandaliwa kwa ufadhili wa Serikali ya watu wa Japan kupitia Shirika la Misaada la JICA (Japan International Cooperation Agency) uliainisha kwamba makutano yanayopaswa kujengwa Barabara zipitazo juu (Fly overs) ni yafuatayo:

i. Makutano ya barabara za Morogoro na Bibi Titi Mohamed
ii. Makutano ya barabara za Morogoro na United Nations
iii. Makutano ya barabara za Morogoro na Kawawa
iv. Makutano ya barabara za Morogoro na Mandela
v. Makutano ya barabara za Nyerere na Msimbazi
vi. Makutano ya barabara za Nyerere na Kawawa
vii. Makutano ya barabara za Nyerere na Mandela

viii. Makutano ya barabara za New Bagamoyo na Kawawa
ix. Makutano ya barabara za Bagamoyo na Sam Nujoma
x. 10 Makutano ya barabara za Kilwa na Mandela

Serikali inajipanga katika kutekeleza mpango huo kwa awamu tofauti tofauti kulingana na uwezo wa kifedha

Aidha kabla ya Uhuru hali ya Miundombinu ya Mawasiliano ilikuwa duni sana. Hakukuwepo na mawasiliano ya simu, Redio wala Televisheni, sasa kuna Televisheni, Simu za mkononi, Fax, e-mail na Radio za masafa yote.

ARDHI MIPANGO NA MAZINGIRA
ARDHI, UPIMAJI WA MIPANGOMIJI
ARDHI

Kabla ya Uhuru sheria za Ardhi zilizotawala miliki ya Ardhi ilikuwa 'Free hold' iliyoridhiwa kutoka kwa wakoloni. Baada ya Uhuru, miliki ya Ardhi ilibadilika na kuwa 'Certificate of Occupancy' ambapo Ardhi nayo ilikuwa mali ya Umma.
Fidia ililipwa kwa maendelezo juu ya Ardhi na sio thamani ya Ardhi tupu. Baada ya mwaka 1999 mabadiliko yalifanywa kwa mujibu wa sheria No 4 na 5 ya Ardhi ya mwaka 1999 na Ardhi kuwa ina thamani.
Sheria na 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 ilijikita zaidi juu ya Ardhi mijini na Sheria 5 ya Ardhi ya mwaka 1999 ilielezea juu ya Ardhi za vijijini.

Umiliki wa Ardhi

Kabla ya Uhuru ni watu wachache ndio waliowezeshwa kumiliki Ardhi ambao wengi wao, walikuwa Wazungu, Wahindi, Waarabu na baadhi ambao walikuwa vibaraka wa wakoloni. Miliki zilikuwa za Kibaguzi na za kitabaka.

Baada ya miaka 50 ya Uhuru maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam yalikuwa yanakaliwa na wazawa ambapo maeneo mengi kati ya eneo la kati la biashara (CBD) Kariakoo, Ilala, Magomeni yamekuwa yakiuzwa kwa watu wenye uwezo wa maendelezo ya majengo ya ghorofa.

Utoaji wa miliki za Ardhi umekuwa ukitolewa kwa kasi na kwa kutumia TEKNOHAMA ikilinganishwa na miaka kabla ya Uhuru hadi miaka ya 1999.

Baada ya miaka 50 ya Uhuru sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 namba 4 na 5 Ardhi imekuwa ikitumika na thamani katika miaka 50 ya Uhuru ni wazi kuwa thamani ya utwaaji Ardhi imekuwa ni ghali ikilinganishwa na wakati kabla ya Uhuru.

Miaka ya mwanzo kabla na baada ya Uhuru hadi miaka ya 1990 viwanja vilikuwa vinatolewa bure na mamlaka husika ila gharama ndogo za upimaji na uandaaji hati ndizo zilizolipwa. Halmashauri nyingi ikiwemo ya Dar es Salaam zilikuwa hazina uwezo wa kifedha kupima viwanja ikilinganishwa na idadi ya maombi ya viwanja iliyotolewa. Hali hiyo ilisababisha ukuaji wa makazi holela.

Uzoefu wa Miaka 50 ya Uhuru ni kuwa viwanja vimeanza kuuzwa kutokana na upandaji wa gharama za utwaaji, upimaji na uandaaji miliki ya viwanja baada ya sheria namba 4 ya Ardhi ya mwaka 1999 kuanza kutekelezwa.

Kabla ya Uhuru, watu wa kipato cha chini walikuwa wanaishi mitaa iliyokuwa duni yenye msongamano mkubwa (Magomeni, Ilala na Temeke Government Quarters)

Maeneo ya Viwanja vya masafa ya chini (Low Density Plot) yalijulikana kama Uzunguni, masafa ya kati yakiwa Uhindini na masafa ya juu (High Density) kwa wananchi wa kipato cha chini. Miliki ya viwanja vya masafa ya chini Low Density ni miaka 99, kwa viwanja vya masafa ya kati miaka 66 na miaka kwa viwanja vya masafa ya juu kuwa miaka 33. Hati za muda zilitolewa na baadaye hati za kudumu.

UPIMAJI ARDHI NA RAMANI

Kabla ya Uhuru hakuna eneo katika Jiji la Dar es Salaam lililoendelezwa bila kupimwa kulingana na sheria ya upimaji. Mamlaka ya Jiji la Dar es Salaam ziliweza kupima viwanja vya kutosha kulingana na maombi yaliyokuwepo. Fani ya upimaji na Ramani imekuwa ikifanya kazi yake ipasavyo. Baada ya Uhuru Mji wa Dar es Salaam ulikuwa kwa kasi zaidi kuliko uwezo wa Halmashauri ya Jiji wa kupima viwanja.

Kati ya miaka 1999 -2006, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilichukua mikakati ya kupima viwanja katika mradi ya viwanja Elfu Ishirini. Viwanja zaidi ya 45,000 vilipimwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji. Mradi huu kwa sasa umehamishiwa kwenye Halmashauri za Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke kuanzia mwaka 2008.

Halmashauri zimekuwa na jitihada mbalimbali za kupima viwanja lakini kutokana na uwezo mdogo wa kifedha imewawia vigumu hususan katika utwaaji wa maeneo kwa ajili ya upimaji viwanja.

MIPANGOMIJI NA UDHIBITI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI

Mamlaka ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa na mpango wa matumizi ya Ardhi hata kabla ya Uhuru ambapo maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali yalitengwa. Aidha, kuongezeka kwa uhitaji wa viwanja na kupungua kwa uwezo wa Mamlaka za Jiji kupata viwanja vilivyopimwa yalisababisha makazi holela kuongezeka. Sheria ya Mipangomiji zilizokuwepo kutoka mwaka 1956 na kutungwa upya mwaka 1961 na baadae kufanyiwa marekebisho 2007 katika sheria hizi zimebainisha mbinu za kuendeleza matumizi ya Ardhi.

Baada ya miaka 50 ya Uhuru Mamlaka za Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam zimekuwa na mikakati mbalimbali ya kuandaa matumizi ya Ardhi, kuendeleza upya maeneo ya kati, kudhibiti ukuaji holela wa makazi, kurasimisha

makazi holela na kuandaa mpango kabambe wa Jiji. Mpango wa uendelezaji upya na maeneo ya Kariakoo, Upanga, Msasani, Temeke, Ilala, Magomeni umeandaliwa na kuanza kutekelezwa. Ukuaji wa Jiji umefanyika kwa kila upande ukielekea kwenye njia kuu za kuingia katikati ya Jiji kwenye Bandari. Ukuaji huo zaidi ya asilimia 75 ni makazi holela na asilimia 25 ni maeneo yaliyopangwa kimipango miji na kupimwa.

MAENDELEO YA JAMII:

Serikali ina jukumu la kuwasaidia na kuwahamasisha wananchi ili waweze wenyewe kupanga mipango yao ya kimaendeleo ikiwemo kubuni miradi ya maendeleo na kuwa na umiliki nayo na kuitekeleza ili kujiletea maendeleo yao.

VIKUNDI VYA KIUCHUMI VYA WANAWAKE

Kimkoa kuna jumla ya vikundi 3,958 vya kiuchumi vya wanawake ambapo vinajishughulisha na shughuli za kiuchumi.

USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA KUPIGA VITA UMASKINI

Mkoa unatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na wanawake katika kukuza pato la Taifa. Kimkoa inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya wananchi walio kwenye sekta isiyo rasmi ni wanawake ambao wamejiimarisha katika shughuli za ujasiriamali. Kumekuwepo na jitihada mbalimbali zinazofanywa Kimkoa katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, kama ifuatavyo:-

(a) Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi

Mfuko huu ulianza kutoa mikopo mwaka 2007 kupitia benki za NMB na CRDB. Kiasi cha fedha kilichotengwa kukopeshwa kwa wananchi ni Tshs Bilioni 3, ambapo zilizokopeshwa ni Tshs. 3,522,000,000 sawa na asilimia 117.4 ya fedha zilizoidhinishwa. Mafanikio yaliyopo ni kwamba jumla ya wananchi 3,097 wakiwemo wanawake 1,852 na wanaume 1,245 walinufaika. Hali ya urejeshaji mikopo ni nzuri

(b) Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake

Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kuwasaidia wanawake na vijana kujikwamua kiuchumi kupitia mikopo kwa vikundi. Jumla ya Tshs 716,947,679 zilitolewa na kukopeshwa vikundi. Hata hivyo, utaratibu huu hautumiki tena badala yake wananchi na vikundi vimeendelea kukopa kupitia Benki ya Wananchi wa Dar es salaam. Katika Benki hii Halmashauri zimekuwa zikichangia fedha kwa ajili ya kukopesha vikundi vya kiuchumi. Kiasi cha fedha kilichokwisha kutolewa na Halmashauri ni Tshs. 1,487,000,000.

Aidha, Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2007 Mkoa ulipatiwa jumla ya T.shs 16,000,000 kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza wanawake kiuchumi. Jumla ya vikundi 26 vilikopeshwa.

Michango Mingine kutoka kwa Wadau Mbalimbali

Vikundi vya kiuchumi katika Mkoa huu vimewezeshwa kupata misaada mbalimbali iliyofadhiliwa na Serikali kupitia mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF), TACAIDS na mradi wa MACEMP. Vikundi 59 vya makundi maalum vimepatiwa mitaji ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi. Jumla ya fedha Tshs 303,472,843 zimetolewa.

MAFANIKIO

Wananchi katika Mkoa huu wanayo mafanikio ya maendeleo ya kujivunia kutokana na uwezeshwaji kutoka Serikali na wadau. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na:-

i. Elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa miradi inaendelea kutolewa zaidi kwa wanawake ili washiriki kikamilifu katika uchumi.
ii. Baadhi ya watu wameinuka kiuchumi kutokana na mikopo waliyopata na kuwawezesha kuanzisha miradi mingi ya kuboresha afya za familia zao
iii. Kuna ongezeko la taasisi za kifedha (PRIDE, PTF, FINCA, VIKOBA n.k) zinazotoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya kiuchumi.
iv. Maonesho ya sabasaba, juakali na mengineyo yamekuwa fursa na yamewezesha wajasiriamali wengi kupata soko la bidhaa zao

v. SACCOS 2 za Wanawake TAWESACCOS na MVIMWATE zenye jumla ya wanachama 4,300 zimeanzishwa

vi. Benki ya wanawake imeanzishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam

CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio hayo kuna baadhi ya changamoto ambazo zinawakabili wananchi wa Dar Es Salaam katika juhudi zao za kujiletea maendeleo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Mabenki na taasisi za kifedha bado zinatoza riba kubwa kwa wakopaji. Hivyo, vikundi vilivyo vingi hushindwa kutimiza masharti na hivyo hukwama katika upanuzi wa miradi yao.

ii. Wafanyabiashara ndogo ndogo wengi bado wanahitaji elimu juu ya ufungashaji wa bidhaa ili kukuza soko la bidhaa zao

iii. Uhaba wa maeneo rasmi ya kufanya biashara kwa vikundi vidogo vidogo

i. Baadhi ya wanavikundi waliokopeshwa kutokuwa na maeneo ya kudumu

ii. Kuendelea kushawishi wawekezaji wa ndani na nje ili wawekeze katika miradi itakayoinua vikundi vya kiuchumi

iii. Kuendelea kuchangia Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam ili kuwezesha vikundi vingi vya kiuchumi kupata mikopo

iv. katika maeneo waliyopatiwa mikopo, hali hii husababisha baadhi ya wakopaji wasio waaminifu kuhama bila taarifa na hivyo kusababisha ufuatiliaji wa marejesho kuwa ngumu.

Wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wataendelea kujiunga katika vikundi na kuibua miradi mbalimbali Serikali na wadau wengine wa maendeleo wataimarisha juhudi za kusaidia shughuli hizo kupitia uwezeshaji wa Serikali katika kuwapatia wananchi maendeleo endelevu.

UKIMWI

Ukimwi ni janga la Kitaifa ambalo mgonjwa wa kwanza katika Mkoa wa Dar es Salaam alipatikana mwaka 1984. Utafiti uliofanyika mwaka 2007/2008 ulionesha kiwango cha maambukizi katika Mkoa kuwa asilimia 9.3% ambayo ni zaidi ya wastani wa kiwango cha taifa cha asilimia 5.7%.

Wananchi wamehamasishwa kupima afya zao ili kuchukua hatua za kimipango ya maisha. Wananchi waliopima afya zao ni 348,491 na waliobainika kuambukizwa ni 23,256 sawa na asilimia 6.7. Waathirika ambao wanatumia dawa za kurefusha maisha ni 21,918. Msisitizo mkubwa unawekwa katika kubadili tabia.

JINSIA

Jinsia ni mahusiano ya kijamii yanayotambua wavulana na wasichana, wanawake na wanaume wamelelewa katika misingi

tofauti kufuatana na tabia, mila, desturi, utamaduni na matarajio ya jamii husika. Mahusiano ya kijinsia yanajengwa kwa njia ya kuelekeza au kufundisha makuzi na malezi au kwa mtu kujifunza. Kwa hali hiyo, mahusiano ya kijinsia yaliyojengeka vilevile yanaweza kubadilika au kubadilishwa kutokana na mazingira.

Masuala ya Jinsia Mkoani Dar es Salaam

Masuala ya Jinsia Mkoani Dar es Salaam ni mwendelezo wa jitihada nyingi zilizofanyika katika kumkomboa mwanamke katika wimbi la ubaguzi, unyanyasaji, na ukandamizaji. Ubaguzi wa kijinsia uliibua mapungufu ya kijinsia katika maendeleo ambayo yanatokana na tofauti kati ya wanawake/wasichana na wanaume/wavulana zilizojengwa kwanye mila na desturi na sheria tangu kuanzishwa kwa Mkoa mnamo mwaka 1973 hadi sasa 2011 tunaposheherekea miaka hamsini ya uhuru wa Tanzania Bara.

Ili kurekebisha hali hiyo, kulikuwa na dhana ya wanawake na maendeleo ambapo mkazo zaidi ulikuwa kuwakomboa wanawake kiuchumi na kifikra bila kumshirikisha mwanaume. Dhana ya Jinsia na maendeleo inasisitiza mahusiano kati ya wanawake na wanaume katika kuboresha maisha ya wote kwa pamoja.

Ushirikishwaji wa wanawake katika maamuzi ndani ya Mkoa.

Kuhusu ushirikishwaji wanawake katika maamuzi mbalimbali ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, Halmashauri na Kata / Mitaa imekuwa ikiwaelimisha wanawake kwa kuwajengea uwezo wa kuongoza vikundi vya kiuchumi kwa kuhakikisha kuwa kila kikundi cha kiuchumi lazima kiwe na Mwenyekiti wa Kikundi, Katibu wa Kikundi, Mhasibu na Wajumbe. Suala hili, limeongeza ari ya wanawake Mkoani katika kugombea nafasi mbalimbali za Uongozi ngazi ya Ujumbe na Wenyeviti katika ngazi ya Kijiji na Mitaa.

Wanawake pia wanashika nafasi nyeti katika Mkoa na Wilaya kwenye eneo la kufanya maamuzi. Katika vipindi vitatu tofauti Mkoa umeongozwa na wanawake katika nafasi ya Katibu Tawala wa Mkoa. Kuhusu Wakuu wa Wilaya mwanamke ni mmoja kati ya nafasi 3. Pia, katika nafasi za Makatibu Tawala Wasaidizi wanawake ni wawili kati ya nafasi sita(6), Makatibu Tawala wa Wilaya wanawake ni wawili kati ya nafasi 3, na Wakuu wa Idara ya Mipango na Uratibu katika Halmashauri zote nne wanawake ni 3 kati ya nafasi 4 za Wakuu wa Idara hiyo. Aidha, kwa ujumla wake Wakuu wa Idara zote katika Halmashauri wanawake ni 10 kati ya nafasi 30. Hii inaonesha jinsi wanawake wanavyoshiriki katika maamuzi mbali mbali ndani ya Serikali Mkoani Dar es Salaam.

Mafanikio katika kuwawezesha wanawake na wanaume ndani ya Mkoa.

Baada ya uhuru mwaka 1961 na kufuatia kuanzishwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam mnamo mwaka 1973, Mkoa unatambua mchango mkubwa wa Wanawake katika kuendeleza familia na kukuza pato la kaya. Katika kuendelea kufanikisha suala hili, Mkoa umesisitiza uanzishwaji wa vikundi na utoaji wa Elimu kwa Wajasiriamali.

Hadi sasa mwaka 2011, vikundi vya kiuchumi vya Wanawake 5,730 na Wanaume 2,455 vimeanzishwa. Shughuli ambazo vikundi hivi vinafanya ni uuzaji wa vyakula, ususi, ufumaji, uhunzi, usindikaji na ufungashaji wa bidhaa mbalimbali. Vilevile, uhamasishaji Wanawake kujiunga katika Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) umefanyika katika Kata 90 ndani ya Mkoa. Mitandao 3 na SACCOS 5 za Wanawake zimeanzishwa. Aidha, vikundi 134 vya kiuchumi vya Wanawake vimeshiriki katika maonesho ya kimataifa ya biashara.

Wanawake na wanaume wamekuwa wakifaidika na kuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira, maarufu kama Mabilioni ya JK iliyowezesha kwa kiwango kikubwa kukwamua jamii katika hali ya kiuchumi.

Katika miaka mitano ya awali ya Uongozi wa Awamu ya Nne tumeshuhudia ndoto ya muda mrefu ya kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake nchini ikitimia ambayo makao yake makuu ni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi kufikia tarehe 28 Februari 2011 mtaji wa benki hiyo ulifikia kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 4.8. Benki hii imekuwa ikitoa mikopo kwa ajili ya mitaji ya kuendesha biashara pamoja na mahitaji ya binafsi kwa wateja wake mbalimbali ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa mingine ya Tanzania. Benki imeshatoa mikopo kwa wanawake na wanaume yenye thamani ya shilingi billioni 8.4 ambapo wanawake ni 3,862 sawa na asilimia 81 na wanaume 855 sawa na asilimia 18. Benki hii tofauti na benki zingine hutoa mafunzo kwa wateja wake na imeshatoa mafunzo kwa wanawake wajasiriamali wapatao 5,668.

CHANGAMOTO

Changamoto kubwa ambayo imekuwa ikiikabili jamii ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam ni ukatili dhidi ya wanawake, watoto na Albino. Serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa ya kutokomeza ukatili huu ambao umejikita zaidi katika mila na desturi za jamii. Katika kufanikisha azma hii, suala hili limekuwa likishughulikiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa na Halmashauri za Serikali za Mitaa ambapo mipango hii imejikita katika kutekeleza mambo mbalimbali yakiwemo:-

i. Kuendeleza kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia iliyoizindua mwezi Mei, 2008 kwa kuelimisha jamii kupiga vita ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na mauaji ya Albino, kwa kutumia filamu maalum iliyoandaliwa.
ii. Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji (2001-2015) hapa nchini, unaotekelezwa na wadau mbalimbali.
iii. Kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria 274 wakiwemo Polisi, Askari wa Magereza, Mahakimu na Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji.

HITIMISHO:

Ndugu Wananchi,

Tunaposherehekea miaka 50 ya Uhuru Mkoa wa Dar es Salaam umekumbana na changamoto nyingi zinazotokana na kukua kwa haraka kwa Jiji la Dar es Salaam. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:

1. Ongezeko kubwa la watu kuingia Jijini kusikowiana na huduma zilizopo
2. Ongezeko kubwa la idadi ya magari yanayoingia nchini na kubaki Jijini Dar es Salaam kusikowiana na miundo mbinu ya barabara iliyopo na inayozidi kujengwa hivyo kusababisha msongamano wa magari barabarani.

3. Uzalishaji mkubwa wa taka usiowiana na uwezo wa uondoshaji wa taka hizo kutokana na nyenzo chache na rasilimali zisizotosheleza uondoshaji wa taka hizo
4. Ujenzi holela katika makazi ya watu kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri kutenga na kupima maeneo kwa ajili ya makazi kusikowiana na ongezeko la watu kuhamia Jijini
5. Kuongezeka kwa kasi kwa Wafanyabiashara ndogo ndogo kutoka Mikoani kuingia Jijini kwa ajili ya kutafuta maisha
6. Kuongezeka kwa omba omba na watoto wa mitaani wanaokuja kutafuta maisha

Kutokana na changamoto hizo Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali.